

---

HIV and AIDS

Social and Behavioral Science Research (SBSR)

---

2014

## **Kuongeza ushahidi unaojulikana kwa kuzuia maambukizi ya Virusi vya UKIMWI (VVU) mionganini mwa wasichana na wanawake [Scaling up evidence-informed HIV prevention for adolescent girls and young women]**

Melanie Croce-Galis

Karen Hardee

Jill Gay

Follow this and additional works at: [https://knowledgecommons.popcouncil.org/departments\\_sbsr-hiv](https://knowledgecommons.popcouncil.org/departments_sbsr-hiv)  
**How does access to this work benefit you? Let us know!**

---

### **Recommended Citation**

Croce-Galis, Melanie, Karen Hardee, and Jill Gay. 2014. "Kuongeza ushahidi unaojulikana kwa kuzuia maambukizi ya Virusi vya UKIMWI (VVU) mionganini mwa wasichana na wanawake [Scaling up evidence-informed HIV prevention for adolescent girls and young women]," What Works brief. Washington, DC: Population Council and What Works Association, Inc.

This Brief is brought to you for free and open access by the Population Council.

Juni 2014



## KUONGEZA USHAHIDI UNAOJULIKANA KWA KUZUIA MAAMBUKIZI YA VIRUSI VYA UKIMWI (VVU) MIONGONI MWA WASICHANA NA WANAWAKE

### *Muhtasari*

Melanie Croce-Galis,<sup>1</sup> Karen Hardee,<sup>2</sup> na Jill Gay<sup>1</sup>

<sup>1</sup> Muungano wa What Works, <sup>2</sup> Baraza la Kutathmini idadi ya watu

Picha kwa Hisani: 2006 Mike Wang/PATH, Fadhila ya Photoshare

### I. Utangulizi

Vijana wa sasa walio katika umri wa kubaleghe, hawauji ulimwengu usiokuwa na VVU.<sup>1</sup> Watu wanaozaliwa wakiwa na vurusi nya UKIMWI na wale ambao wanaanza kushiriki ngono katika enzi hizi za Virusi nya UKIMWI (VVU) na UKIMWI, wanakumbwa na hatari halikadhalika changamoto ambazo hazikuwepo katika vizazi viliviyotangulia. Leo hii, vijana bilioni 1.8 wenye umri kati ya miaka 10 na 24 wanaunda asilimia 26 ya idadi ya watu ulimwenguni. Katika maeneo mengine, kwa mfano, kusini mwa jangwa la Sahara wakiwakilisha asilimia 32.2.<sup>2</sup> Mataifa mengi yenye idadi kubwa ya watu walioambukizwa VVU yanashuhudia ongezeko ghafla la idadi ya vijana. Hivyo basi, hata idadi ya maambukizi ya VVU yanavyozidi kurudi chini, idadi kamili ya vijana wanaoishi na VVU au walio katika hatari ya kuambukizwa, itaongezeka katika kipindi cha miaka mitano ijayo. Kuna kuongezeka kwa ushahidi ya kwamba tabia hatari mionganoni mwa watu wakazi muhimu huanza katika umri wa kubaleghe.<sup>3</sup> Kwa hivyo, vijana katika umri wa kubaleghe wanapaswa kupewa kipaumbele katika mipango ya kuzuia VVU. Hasawanawake vijana wamo hatarani huku viwango nya maambukizi ya VVU mionganoni mwao vikiwa mara mbili zaidi ya mionganoni mwa wenzao wa kiume.<sup>4</sup> Mwisho wa mwaka wa 2012, takribani theluthi mbili ya maambukizo mapya ya VVU mionganoni mwa vijana katika umri wa kubaleghe kati ya miaka 15 na 19, yalikuwa mionganoni mwa wasichana.<sup>5</sup>

#### Kuhusu muhtasari huu

*Muhtasari huu unaotoa kipaumbele kwa utekelezaji ambao imeshuhudiwa kufaulu kwa mipango ya awali ya wanawake na wasichana. Ingawa baadhi ya mipango ya kuingilia kati iliyotajwa pia inawafaidi wanaume na wavulana.*

*Muhtasari huu umegawanywa katika sehemu tatu: ushahidi unaojulikana katika kipaumbele cha utekelezaji; Mapengo ya utekelezaji na utafiti sharti uangaliwe; na masuala ya kuongeza mipango yenye ufanisi mionganoni mwa wasichana na wanawake. Kwa maelezo zaidi kuhusu mipango hii, tazama tovuti, [www.whatworksforwomen.org](http://www.whatworksforwomen.org). Hatua ya kuingilia kati ilivyoelezwa hapa ina msingi tathmini ya kina ya ushahidi ulimwenguni kote; Hata hivyo, kukabaliana kwa kila nchi na jamii inapaswa kuundwa kudhi fursa maalum na changamoto za eneo hilo.*

Kizazi huru kutokana na maradhi ya VVU haiwezekani bila kushughulikia mahitaji maalum ya vijana walio katika umri wa kubaleghe – hasa wasichana- kinacho waweka hatarini ya kuambukizwa VVU.



**USAID**  
FROM THE AMERICAN PEOPLE

 **Evidence**  
 **POPULATION COUNCIL**  
Ideas. Evidence. Impact.



 **WHAT WORKS  
ASSOCIATION**

## Utaratibu

Ushahidi wa ufanisi na wenyе ahadi ya kuzuia VVU mionganі mwa wanawake, ulikusanya kwa mapitio ya maandiko ya "What Works for Women and Girls: Evidence for HIV/AIDS Interventions" ([www.whatworksforwomen.org](http://www.whatworksforwomen.org)) katи ya Januari 2012. Matokeo yalipata msingi kwa mikutano na wataalamu wanaongoza katika utafiti, sera, na mipango ya vijana walio katika umri wa kubaleghe, pamoja na utafiti uliofanywa kwa kutumia SCOPUS, Medline, na Popline katи ya mwaka wa 2005 hadi 2011, kwa kutumia maneno "VVU," "UKIMWI," "Wanawake," na maneno mengine mahususi. Maandiko ya Gray yalipatikana kuitia uchunguzi upya wa tovuti muhimu mionganі mwao mashirika ya Umoja wa Mataifa, Shirika la Afya Ulimwenguni, Ushirikiano wa Cochran; Taasisi ya Open Society; Baraza la Kimataifa kuhusu Utafiti wa Wanawake; Baraza la Idadi ya Watu; Muungano wa Kimataifa wa Wanawake wanaoishi na UKIMWI, Benki ya Dunia FHI 360; AIDStar I na II, na Taasisi ya Guttmache. Piawataalamu walishauriwa katika kila mada kuhakikisha kuwa ushahidi ulionyeshwa vilivyo (tazama [www.whatworksforwomen.org](http://www.whatworksforwomen.org) kwa maelezo zaidi kuhusi metodolojia, ikiwa ni pamoja na nambari kamili ya makala na ripoti zilizonyeshwa na orodha kamili ya marejeo).

Kupata kiwango cha nguvu za ushahidi, makala yaliorekebishwa ya Gray yalitumika (tazama Jedwali 1). Haya yaliundwa kwa matumizi ya uchunguzi wa kiutaratibu

chini ya "The Cochrane Collaboration of systematic reviews" (<http://www.cochrane.org/>) na kujionyesha yenyewe kwenye aina mbili za mapitio haya. Mbinu hii inashirikisha vipimo vitatu ili kupanga kuingilia katи "Inayo fanya kazi" na "iliyo na ahadi:"

1. Kina cha ushahidi (ni tathmini/ tafiti ngapi zinazosaidia mpango huu wa uingiliaji katи);
2. Upana wa ushahidi (ni nchi ngapi zinazochangia ushahidi kusaidia mpango wa kuingilia katи); na
3. Uthabiti wa ushahidi (Mizani ya Gray), ambapo "Kinachofaa" kinahusisha utafiti wa Gray I, II, au IIIa kwa anagalau nchi mbili na/au utafiti wa Gray IIIb, IV tano, au V katika mataifa zaidi ya moja, na "Kinachoonyesha matumaini" kinahusisha tafiti I, II, au IIIa za Gray katika mandhari mojawapo ya angalau tafiti mbili zilizotathiminiwa kama Gray IIIb, IV, au V katika nchi au eneo moja.

Ushahidi huu uligawanywa kwa kutumia mfano wa kijamii na ikolojia (tazama Picha 1) na kuratibiwa zaidi na vijana katika umri wa kubaleghe kutoke sehemu mbali mbali. Kwa kiwango fulani, vitengo hivi vyaweza kubadilishwa. Kwa mfano, huenda kanuni za kijinsia zikaangaziwa katika kiwango cha jumuiya na kijamii; mipango ya kielimu iliyolengewa watu yaweza angaziwa katika kiwango cha jumuiya au kijamii, n.k. Kwa hivyo, kutunga hii ni kwa minajili ya kutoa mfano.

### Jedwali 1. Mizani ya Gray ya Nguvu za Ushahidi

Aina	Nguvu za Ushahidi
I	Ushahidi thabiti kutoka kwa angalau ukaguzi mmoja wa majoribio kadha yaliyosanifiwa vyema bila kudhibitiwa.
II	Ushahidi thabiti kutoka kwa angalau jaribio moja la kesi iliyothibitiwa, usio na mapangilio na yenye ukubwa sahihi.
IIIa	Ushahidi kutoka kwa majoribio yaliobuniwa vyema/masomo bila kubahatisha na inayohusisha vikundi vya kudhibiti (kwa mfano, nusu-majoribio, yanayoambatana na masomo ya majoribio, kabla ya wadhifa na kikundi kinachothibitiwa).
IIIb	Ushahidi kutoka kwa majoribio yaliyobuniwa vyema/masomo bila ubahatishaji inayohusika na vilivydhibitiwa (kwa mfano; kikundi moja kabla ya wadhifa, kundi, muda usio na mfululizo).
IV	Ushahidi uliobuniwa vyema, masomo ambayo isio ya majoribio kutoka kwa zaidi ya kikundi kimoja cha utafiti.
V	Maoni kutoka walio na mamlaka yanayoheshimika kuambatana na ushahidi wa kimatibabu, masomo ya kimaelezo, au ripoti za baraza la wataalamu.

**Fahamu:** Gray inahusisha aina tano za ushahidi unaojulikana.<sup>6</sup> Kwa kile kinachofanya kazi, kiwango III kimegawanywa zaidi kutofautisha katи ya masomo ya ubora na tathmini zinazojumuisha makundi yaliodhibitiwa (IIIa) na zile zisizofanya hivyo (IIIb). Masomo ya ubora yaangukia viwango mbili IV na V, kulingana na idadi ya washiriki kwenye masomo ya ubora na sababu zingine.<sup>7</sup>

## Kanuni Elekezi za Utaratibu wa Vijana Katika Umri wa Kubaleghe

Kwa sababu umri wa kubaleghe ni kipindi cha kuchagiza, mbinu yenyе mabadiliko ya kijinsia – inayonua kubadilisha mahusiano ya kijinsia ili kuimarisha usawa kama mbinu ya kuafikia matokeo ya kiafya<sup>8</sup> – ni muhimu kuwepo kwa mipango kuhusu vijana wanaobaleghe. Kwa sababu inaweza kushughulikia madhara kanuni ya kijinsia inayowaweka wanawake katika hatari ya kuambukizwa VVU.

Mipango ya vijana wanaobaleghe ni lazima yaambatane na kanuni za haki za kibinadamu, kama yalivyoanishiwa kwenye mkataba wa haki za kibinadamu na mikataba mingine, ikiwa ni pamoja na Mapatano Kuhusu Haki za Mtoto.<sup>9</sup>

Ni muhimu kufahamu kuwa kiwango kikubwa cha ushahidi uliotajwa hapa Kimetokana na tafiti ambazo zimefanywa miiongoni mwa wale ambao hawakuhitaji idhini kutoka kwa wazazi ili kushiriki, umri wa miaka 18 katika nchi nydingi, lakini huenda ikatofautiana—umri unaohitaji idhini unategemea uamusi wa bodi ya nchi kiasisi cha kuhakiki ya kila nchi. Hata hivyo, kazi nydingi zinazofanywa kwa watu wazima, kama kuongeza juhudzi za kushauri na kupimwa VVU, zaweza okoa maisha ya vijana katika umri wa kubaleghe. Ijapokuwa sio masomo yote ambao yametajwa yalifanywa miiongoni mwa vijana wanaobaleghe (vikundi vya umri vimeonyeshwa), baadhi ya matokeo yaweza tumiwa na utathmini kali inayotumika miiongoni mwa vijana wanaobaleghe. Vivyo hivyo, ushahidi unaojulikana kwa kuongeza kuingilia kati, unaambatana na uzoefu na

kuongeza mipango ya umri zote. Ijapokuwa uzoefu maalum kwavijana wanaobaleghe ungali unaibuka.<sup>10</sup> Tathmini ya kuendeleza mipango kuhusu vijana itasaidia kuziba mapengo katika ushahidi uliopo kwenye mipango ya kuzuia VVU miiongoni mwa vijana.

## II. Mipango ya kuingilia kati iliopewa kipaumbele

Kutokana na ushahidi unaojulikana kufikia sasa, mipango ya kuingilia kati iliyoordheshwa hapa chini inapaswa kupewa kipaumbele kwa kuzuia VVUmiiongoni mwa vijana wanaobaleghe. Vipengele muhimu katika utekelezaji vimeandikwa kwa herufi za mlazo na mitajo ya kuihimili kubainishwa. Ingawa kuna mipango mingi mingine iliyo na matumaini, imebakia mipango michache iliyofanyiwa utathmini itakayowawezesha vijana kuhalalisha mapendekezo ya kuimarishwa kwa viwango vya kitaifa. Mashauri mawili makuu ni kuongeza viwango vya elimu kwa vijana katika umri wa kubaleghe na kutoa elimu bora na ya kina kuhusu masuala ya ngono.

**Kumbusho kuhusu umri:** Mahitaji ya vijana walio katika umri wa mapema wa kubaleghe (miaka 10 hadi 14), yanatofautiana pakubwa na ya vijana walio katika umri wa mwisho wa kubaleghe (miaka 15 hadi 18), na vijana wanaokaribia utu uzima (miaka 19 hadi 24). Kwa hivyo, mapendekezo yafuatayo pamoja na vijenzi vyake vinapaswa kutekelezwa katika mbinu zinazoambatana na umri wao. Hata hivyo, tabia zinazohusu ngono miiongoni mwa vijana wanaobaleghe hazina mipaka ya kiumri: kuna baadhi ya vijana wanaobaleghe ambao huenda wakaanza kucheza ngono mapema, huku wengine wakingojea mpaka wawe wa umrimkubwa.

Picha 1: Mfano wa Muundo wa Kijamii na Ikolojia






Photo by: Star for Life

## Kiwango Cha Kijamii

### ***Kinachofaa: Kuongeza Kiwango cha Elimu kwa Vijana wote Wanaobaleghe***

Kuongeza kiwango cha elimu mionganini mwa wavulana na wasichana kunaweza kusaidia kupunguza hatari ya maambukizo ya VVU. Kuna ushahidi thabiti wa upungufu wa hatari ya maambukizi ya VVU mionganini mwa walioelimika zaidi—hasa wasichana.<sup>11</sup> Mipango a kuingilia kati iliyofaulu kuongeza viwango vya elimu na imehusika kwa kupunguza VVU, ni pamoja na *kuondoa malipo ya karo ili kuwawezesha wasichana kuijunga (au kusalia) shulenii*,<sup>12</sup> na *kutoa usaidizi wa kielimu mionganini mwa mayatima*.<sup>13</sup> *Uhamishaji wa fedha kwa masharti nni mkakati wenye matumaini ya kuwawezesha wasichana kusalia shulenii na hivyo kupunguza maambukizi ya VVU*.<sup>14</sup>

Mikakati ya kupambana na VVU inapaswa kuendeleza elimu kwa wasichana. Kuongeza viwango vya elimu kunahitaji ushirikiano mionganini mwa sekta za afya na elimu. Vile vile, mashirika ya kuratibu mipango ya utekelezaji, ufuatiliaji na utathmini. Ulimwengu mzima, mafanikio yamefikiwa katika kuongeza vijana wanaobaleghe waokamilisha elimu ya msingi. Lakini imekuwa changamoto kuhakikisha vijana wote wanaokamilisha elimu ya upili. Lengo hili ni muhimu lenyewe na linapaswa kufuutiliwa kutohana na uhusiano wake na matokeo bora ya kiafya, ikiwa ni pamoja na upungufu kwa matukio ya VVU.

### ***Kinachofaa: Kutoa Elimu Bora Na Ya Kina Kuhusu Masuala Ya Ngono Mionganini Mwa Vijana Wanaobaleghe***

Kuna ushahidi unaojulikana na uendelevu wa kina unaohusisha elimu ya ngono na masuala ya VVU wenye

tabia fulani (kwa mfano, kuzingatia kuzuia maambukizo ya VVU; kushughulikia hali inayoweza kusababisha kucheza ngono bila kinga na kwa uzembe, na jinsi ya kuzuia hii, na jinsi ya kujiepusha na hali kama hii; kuzingatia maarifa, maadili, itikadi, kanuni, mitazamo na ujuzi; matumizi ya mbinu za mafundisho ya kushiriki n.k),<sup>15</sup> kabla ya kushiriki ngono yaweza kuwa na ufanisi kupunguza unyanyapaa na kuzua maambukizi ya VVU kwa kuongeza umri wa kushiriki ngono kwa mara ya kwanza. Na kwa wale ambao tayari wanajihuisha na ngono, kuongeza matumizi ya kondomu na kupimwa VVU, na pia kupunguza idadi ya watu wanaoshiriki ngono nao.<sup>16</sup> Ni muhimu kutambua kwamba mipango ya kuingilia kati shulenii pekee haijaonesha athari katika kupunguza maambukizo ya VVU, lakini imeonyesha manufaa kuathiri elimu na tabia<sup>17</sup> na kupendekezwa kuwa elimu ya ngono ni muhimu kwa ajili ya kuzuia VVU ufanisi, hivyo kuonyesha umuhimu wa elimu ya masuala ya ngono katika vita dhidi ya maambukizi ya VVU. Lakini inapaswa kuhusishwa na mambo mengine ikiwa ni pamoja na huduma za afya za kirafiki na zinazofikiwa kwa urahisi na vijana.<sup>18</sup>

*Ubora wa elimu ya masuala ya ngono ni muhimu kama riziki yake; uaminifu kwa vipengele na mafanikio ya mipango ya majaribio sharti iimarishwe. Mafunzo ya ziada kwa walimu ili waweze kutoa elimu ya masuala ya ngono kuambatana na umri, elimu ya masuala ya ngono inayowashirikisha wanafunzi na inayoweza kuboresha maarifa yao na ujuzi, ni muhimu.*<sup>19</sup>

Kwa taarifa zaidi, tazama *Elimu ya kina kuhusu masuala ya ngono: Changamoto na Fursa za Kuongeza Viwango* (UNESCO, 2012).

## Kiwango Cha Jumuia

### ***Kinachoonyesha Matumaini: Kuhakikisha ufikiasi wa Huduma za Kiafya na Kupimwa kwa Vijana Wanaobaleghe na WUtu Uzima***

Mara nyingi, mahitaji ya vijana kuhudumiwa hayatiliwi maanani katika shughuli za uundaji wa mipango ya VVU ambayo hajasanifiwa hususan kwa sababu yao. Kwa kutoa huduma za afya zinazokubalika na kufikiwa kwa urahisi na vijana, inayofaa, ya bei nafuu, ya usiri na isiyowahukumu ni mbinu ya kufanikisha matumizi ya huduma za afya ya uzazi, ikiwa ni pamoja na kupimwa na kushauriwa kuhusu VVU (HTC).<sup>20</sup> Sera zinazohitaji idhini ya wazazi ili kuendeleza huduma ya HTC huenda zikawazua vijana wanaobaleghe kufikia huduma. Ushahidi unaojulikana umeonyesha kuwa huduma ya kupimwa na kushauriwa kuhusu VVU,yaweza kusaidia wanawake kujifunza hali yao ya VVU na na hivyo kuungeza tabia za kujikinga kutokana na virusi hivi, hasa mionganoni mwa wanaopatikana na VVU (*inawafaa watu wazima*),<sup>21</sup> Ijapokuwa utafiti mwingi wa kupima VVU hauwalengi vijana wanaobaleghe. Utoaji huduma ya kupima na kushauri kuhusu VVU, pamoja na huduma zingine za kiafya, zimeonekana kuungeza idadi ya watu wazima wanaofikia huduma za HTC (*inafaa mionganoni mwa watu wazima*).<sup>22</sup> Kwa vijana wanaobaleghe na ambao wanaishi na VVU, utoaji wa tiba ya ARVs au madaya yaUKIMWI waweza punguza (*lakini haiondoi kabisa*) hatari ya maambukizi ya VVU. Basi kumaanisha kuwa ni mkakati wa ziada wa kuzuia maambukizi.<sup>23</sup> Kuanzisha itifaki kina ya huduma baada ya kubakwa, ikiwa ni pamoja na kuwapa dawa za kuzuia maambukizi (PEP), pamoja na dawa za dharura za kupanga uzazi, kwaweza imarisha huduma kwa wote.<sup>24</sup>

### ***Kinachoonyesha matumaini: Matumizi ya Vyombo vya Habari na Kampeni za Kijamii za Utangazaji kama ala ya kuwafikia Vijana wanaobaleghe***

Vyombo vya habari na kampeni za kijamii za utangazaji zimekuwa za muhimu katika harakati za kufikia malengo. Zikitumika kwa njia ya umakini na utaratibu pamoja na mipango mingine ya kuingilia kati, zaweza fikia idadi kubwa ya vijana na hivyo kuungeza idadi ya watu binafsi na wapenzi wanaofikia huduma ya kupimwa na kushauriwa kuhusu VVU.<sup>25, 26</sup> Kampeni za aina hii zimekuwa na ufanisi katika harakati za kuwashawishi wasichana na wavulana wanaobaleghe kubadilisha tabia zinazowaweka hatarini mwa kuambukizwa VVU.<sup>27</sup> Ushahidi unaojulikana mionganoni mwa watu wazima umeonyesha kuwa mipango ya kuingilia kati katika jamii (ikiwa ni pamoja na vyombo vya habari) inayotoa habari za kweli kuhusu maambukizi yaweza punguza unyanyapaa dhidi ya wanaoishi na VVU na UKIMWI (*inafaa mionganoni mwa watu wazima*);<sup>28</sup> kampeni za vyombo vya habari kuhusu usawa wa kijinsia kama sehemu ya kina

na inayojumuisha, yaweza kuimarisha tabia za kujikinga kutokana na VVU. (*inafaa mionganoni mwa watu wazima*);<sup>29</sup> na kuimarishwa kwa afya ya umma kwaweza imarisha ufahamu kuhusu dhuluma dhidi ya wanawake (*inafaa mionganoni mwa watu wazima*).<sup>30</sup>

## Kiwango Cha Uhusiano

### ***Kinachoonyesha Matumaini: Kuzingatia Usawa wa Kijinsia kwa Vijana wote Wanaobeleghe na Wanaokaribia Utu Uzima***

Madhara ya kijinsia ni hatari kwa kuambukizwa VVU. Wataalamu wa maendeleo na kijinsia wanazidi kukubaliana kwamba kuingilia kati inayolangazia itikadi za kijinsia na kupunguza maambukizi, inapaswa kuwahuishwa kwa hiari “wanaume na wanawake, wavulana na wasichana, kwa mbinu thabiti itakayokabiliana na itikadi za kijinsia, itakayochochea usawa wa kijinsia na kuimarisha afya.”<sup>31</sup> Kuangazia usawa wa kijinsia katika umri wa kubaleghe ambao ni wa kupata umbo, kwaweza badilisha maishani yote.

Mafunzo kwa walimu kuhusu dhuluma za kijinsia ni mkakati wa kuahidi kubadili kanuni kuhusu kukubaliana kwa tabia hii.<sup>32</sup> Kwa walio katika umri wa juu wa kubaleghe na wanaokaribia utu uzima (umri 16–24),kujifunza mbinu shirikishi ya *kijamii inayowashirikisha wanaume na wanawake* yaweza unda mahusiano zaidi ya usawa wa kijinsia, na hivyo kupunguza vurugu (*inafaa mionganoni mwa watu wazima*).<sup>33</sup> Ushahidi unaojulikana umeonyesha kuwa kuangazia suala la usawa wa kijinsia, hasa mionganoni mwa wanaume (bila umri hususan), kwa *mafunzo, majadiliano baina yao na wenza, na elimu ya kijamii yanayopinga* itikadi mbaya za kijinsia, yaweza kuimarisha harakati za kuzuia maambukizi ya VVU, kupimwa, matibabu, na huduma (*inafaa mionganoni mwa watu wazima*).<sup>34</sup> Mionganoni mwa watu wazima, *mashauriano na mawaidha mionganoni mwa wapenzi*, ikiwa ni pamoja na mbinu za kuzuia dhuluma za kijinsia, pia yaweza ongeza idadi ya wapenzi wanaopokea na kufichua matokeo baada ya kupimwa (*inafaa mionganoni mwa watu wazima*).<sup>35</sup> Hii pia yaweza fanyiwa majaribio kama mbinu kwa wapenzi walio katika umri wa kubaleghe, na vile vile walio katika mahusiano ya mapenzi.

## Kiwango Cha Mtu Binafsi

### ***Kinachoonyesha Matumaini/Kinachofaa: Kuimarisha Ufahamu na Kuhimiza Tabia ya Kujikinga Mionganoni Mwa Wavulana na Wasichana Walio Katika Umri wa Kubaleghe***

Jitihada za kitaifa za kupunguza au kuchelewesha umri wa kujihuisha na kuchenza ngono, kuungeza matumizi ya kondomu, na kupunguza idadi ya watu unaoshiriki ngono

nao ni mbinu thabit za kuzuia maambukizi ya VVU.<sup>36</sup> Baadhi ya mipango ya kuingilia kati yenyen mafanikio ni pamoja na *mipango pana kwa vijana*, kama zile zitumiazo ipengele mbali mbali.

(kwa mfano, sera/utetezi na ushiriakano wa huduma za afya, mafunzo ya ujuzi wa kujiletea mapato, semina, michezo, n.k), yaweza kuboresha ufahamu wa vijana wanaobaleghe kuhusu VVU na kuhimiza tabia za kujikinga (inafaa).<sup>37</sup> Ushauri waweza punguza tabia za kuongeza hatari ya maambukizi ya VVU mionganoni mwa watu wazima,<sup>38</sup> Pia kuhusisha *mijadala kuhusu matumizi ya pombe* kwa shughuli za HTC, kwaweza imarisha tabia ya kujikinga kama vile matumizi ya kondomu, kupunguza idadi ya watu wanaoshiriki ngono nao, na kupunguza matumizi ya pombe (*inafaa mionganoni mwa watu wazima*).<sup>39</sup> Lakini masomo haya hayakufanyiwa majoribio maalum mionganoni mwa vijana wanaobaleghe. Mipango ya uingiliaji kati inayoonyesha matumaini kama vile *kuhimiza mawasiliano baina ya watu wazima na vijana* kuhusu habari za afya ya uzazi, zaweza imarisha tabia za kujikinga mionganoni mwa vijana wanaobaleghe.<sup>40</sup> Pia *elimu kuhusu jinsi ya kujikinga na VVU kutolewa na watu wanaoishi na virusi hivi* (wanaonua kufichua hali yao kupitia kikundi cha watu wanaoishi na VVU kinachopambana na unyanyapaa na ubaguzi) kwa vijana, kwaweza kuhimarisha ujumbe kuhusu tabia za kujikinga.<sup>41</sup>

### ***Kinachoonyesha Matumaini: Kuangazia Mipira ya Kondomu kwa Vijana Wanaobaleghe na Ambao Tayari Wanashiriki Ngono***

Matumizi ya kondomu ni mbinu muhimu ya kuzuia, kupunguza uwezekano wa kuambukizwa VVU kwa zaidi ya asilimia tisini na tano.<sup>42</sup> Matokeo yake yanaweza linganishwa baina ya kondomu za wanaume na wanawake endapo zitatumwi kila mara na kwa njia inayofaa.<sup>43</sup> Matumizi kuanzia mara ya kwanza wanaposhiriki ngono, kufanya kondomu matangazo, kibinasi au katika vikao vya pamoja na mafunzo ya ujuzi, kutoa kondomu, ya *elimu ya kutia hamasa*, kwaweza ongeza matumizi ya kondomu (*inafaa mionganoni mwa watu wazima*).<sup>44</sup> Shughuli za kuimarisha ufikiaji na upatikanaji wa mipira ya kondomu zaweza ongeza matumizi ya kondomu (*inafaa mionganoni mwa watu wazima*).<sup>45</sup> Vile vile, *kupanua shughuli za usambazaji* wa kondomu za kike huenda zikaimarisha matumizi ya kondomu za wanawake na hivyo kuongeza idadi ya watu wanaotumia kinga wanaposhiriki ngono, na hatimaye kuzuia usambazaji na maambukizi ya VVU (*inafaa mionganoni mwa watu wazima*).<sup>46</sup> Kukusa matumizi ya kondomu kati ya watu wawili kama mbinu ya upangaji uzazi na kuzuia maambukizi ya VVU, huenda ukafanya matumizi ya kondomu kukbalika na rahisi kujadili (*inafaa mionganoni mwa watu wazima*),<sup>47,48</sup> hasa kwa vijana (*inafaa mionganoni*



Photo by: hodag

*mwa vijana wanaobaleghe*).<sup>49</sup> Zaidi ya hayo, harakati za usambazaji wa kondomu mionganoni mwa vijana, zaweza saidia vijana wanaobaleghe kuwa na starehe wanapofikia kondomu (*inafaa mionganoni mwa vijana wanaobalehe*).<sup>50</sup> Pia kukuza radhi katika matumizi ya kondomu mionganoni mwa wanaume na wanawake, kwaweza kuongeza mazoezi ya ya kujikinga wakati wa kushiriki ngono (*inafaa mionganoni mwa watu wazima*).<sup>51</sup> Kwa vijana wanaokaribia utu uzima, hatua madhubuti pia ni pamoja na *mawasiliano mionganoni mwa wapenzi* kuhusu hatari ya maambukizi ya VVU, jambo ambalo litaimarisha tabia za kujikinga ikiwa ni pamoja na matumizi ya kondomu (*inafaa mionganoni mwa watu wazima*).<sup>52</sup> Kwa ujumla, kukbalika kwa matumizi ya kondomu mionganoni mwa wanawake na wanaume wanaposhiriki ngono ni mkakati wenye ahadi kupunguza idadi ya maambukizo ya VVU kwa kitaifa.<sup>53</sup>

### ***Kinachoonyesha Matumaini: Wezesha Kuajiriwa Mionganoni Mwa Vijana Wanaokaribia Utu Uzima***

Ijapokuwa kuna haja ya viashirio bora na programu iliooundwa kwa makini ili kupima athari za VVU katika harakati za kuwapa wanawake na wasichana nguvu za kiuchumi, masomo yameonyesha kuwa kuongezeka kwa idadi ya wanawake wanaofikia habari, ujuzi, teknolojia, huduma, usaizidi wa kijamii, na mapato, kuliongeza uwezo

wao wa kujikinga kutokana na maambukizi ya VVU.<sup>54</sup> Kwa wavulana, pia, upatikanaji wa ajira unawezesha ubinadamu mkuu na maaendeleo ya na kijamii pamoja na kuondoa umaskini. Kuongezeka kwa *fursa za ajira, au shughuli ndogo za kuzalisha mapato pia zaweza, punguza tabia zinaongeza hatari ya kuambukizwa VVU*, hasa miiongoni mwa watu wazima, na huenda ikawa na matumaini ya kuleta matokeo miiongoni mwa vijana wanaokaribia utu uzima, iwapo zitatathminiwa kwa makini.<sup>55,56</sup> Upatikanaji kwa urahisi wa vituo vya kupima VVU na kutoa ushauri kazini, huenda kukaongeza idadi ya watu wanaotumia huduma za HTC.<sup>57</sup>

### ***Shughuli: Msaada Kwa Mayatima na Watoto Wanaoishi Katika Mazingira Magumu (OVC)***

Mayatima na watoto wanaoishi kwa mazingira magumu ni wakazi muhimu katika hatari ya kuambukizwa VVU. Mayatima wa kike waliofiwa na wazazi kutokana na UKIMWI, wanakabiliwa na hatari zinazokingamana: Kama watoto, hawana haki za kisheria (kwa mfano urithi na mali), ukomavu, na ujuzi wa kujishughulikia wenyewe. Kama watoto wasichana, hawana fursa sawa za kufikia rasilimali za nyumbani kimasomo, lishe, au kiafya. Janga linapoikumba familia, kwa mara nyingi wasichana ndio hulazimika kukatiza masomo na kuubeba mzigo mkubwa nyumbani. Mafanikio ya mipango ya kuingilia kati kwa mayatima na watoto wanaoishi katika mazingira magumu, ni pamoja na *Ushauri wa Kisaikoloja na Unasihi*, suala ambalo huenda likaimarisha hali yao kisaikoloja.<sup>58</sup> Mipango inayotoa usaidizi wa kiuchumi, kiafya na kijamii kwa familia pia yaweza imarisha matokeo ya kiafya na kielimu miiongoni mwa mayatima.<sup>59</sup> Kwa sababu mayatima hukumbwa na hatari fulani ya maambukizo ya VVU,<sup>60</sup> mipango inayotoa huduma za kijamii za uhamishaji fedha, fursa za biashara ndogo, malipo ya uzeeni au *usaidizi mwengine wa kifedha na mapato uliolengwa*, waweza saidia mayatima vilivyo.<sup>61</sup> Mikakati yenye matumaini ya kuleta matokeo mema kwa mayatima na watoto wanaoishi katika mazingira magumuni pamoja na *miradi ya maendeleo ya jamii*, badala ya mpango uliofanuliwa kwa wembamba usio na kina cha kukabiliana na unyanyapaa dhidi ya mayatima walioachwa kutokana na maradhi haya.<sup>62</sup>

### ***Kinachoonyesha Matumaini/Kinachofaa: Kuwasaidia Vijana wa Kike Wanaoshiriki Kwenye Biashara ya Ngono kujikinga***

Ingawa huenda wanawake wakajingiza katika biashara ya ngono katika umri mdogo, "Umoja wa Mataifa umeweka mipaka kwa kufafanua kazi hii kwa watu wazima kwa zaidi ya miaka 18, na inasisistiza kuwa kuhusika kwa watoto (chini ya miaka 18) katika biashara hii na aina nyingine ya ukandamizaji na dhuluma inayokiuka mapatano ya Umoja

wa Mataifa na Sheria zingine za kimataifa kuhusu haki ya kibinadamu. Watoto chini ya miaka 18 wanaouza ngono ni waathiriwa na kamwe hawawezi chukuliwa wafanyi kuwa wafanyi biashara ya ngono."<sup>63</sup> Harakati za kupambana na maambukizi ya VVU kwa watoto wanaokandamizwa na kutumiwa katika biashara ya ulangizi wa watoto, zilikuwa Zaidi ya upeo wa tathmini hii.

Kwa wanawake zaidi ya miaka 18 wanaojihusisha na biashara ya ngono, kuna baadhi ya mipango ya kuingilia kati ambayo imeonyesha ishara ya kuwa na mafanikio, ikiwa ni pamoja na mipango kina ya kujikinga kutokana na VVU, inayojumuisha na vipengele kama vile elimu ya rika sawa, kutoa huduma na vifaa vya kiafya pamoja na vikundi vya kusaidiana. Hii yaweza kuwa na matokeo katika harakati za kuwasaidia wafanyi biashara ya ngono kuiga mazoea ya ngono salama (inafaa miiongoni mwa watu wazima).<sup>64</sup> *Elimu yaya rika miiongoni mwa wafanyi biashara wa ngono.*<sup>65</sup> (inafaa miiongoni mwa watu wazima). Sera zinazowahusisha wafanyibiashara ya ngono, wamiliki wa madanguro, na wateja maendeleo na utekelezaji wa matumizi ya kondomu, waweza ongeza kuripoti kwa matumizi ya mipira ya kujikinga (inafaa miiongoni mwa watu wazima).<sup>66,67</sup>

Mbinu zingine zenye matokeo ni pamoja na *mipango ya kuingilia kati kimatibabu inayohusisha wafanyi kazi ya uenezi*, ambayo inaweza ongeza ufanisi katika kuongeza matumizi ya kondomu na huduma za kupimwa VVU miiongoni mwa wafanyibiashara ya ngono (inafaa miiongoni mwa watu wazima);<sup>68</sup> *kutoa huduma bora, za usiri na za kila mara za kupimwa maradhi ya zinaa, zinazohusisha kutangaza umuhimu wa matumizi ya kondomu, zaweza punguza hatari ya maambukizi ya VVU miiongoni mwa wafanyibiashara ya ngono* (inafaa miiongoni mwa watu wazima);<sup>69</sup> na kujenga hisia za kijamii, uwevezaji na uongozi miiongoni mwa wanabiashara wa ngono, kwaweza kusaidi kwa ufanisi kuzuia maambukizo ya VVU (inafaa miiongoni mwa watu wazima).<sup>70</sup> Kuwalenga wateja wa kiume ni kuingilia kati kwenye ahadi ya kuongeza matumizi ya kondomu na hivyo kupunguza hatari ya maambukizi ya VVU miiongoni mwa wafanyibiashara ya ngono.<sup>71</sup>

### ***Kinachoonyesha Matumaini: Kuhimiza Tabia ya Kujikinga kwa Vijana Wanaojidunga Dawa za Kulevy***

Katika maeneo ambayo matumizi ya madawa ya kulevy yanachangia kwa janga la VVU, hasa miiongoni mwa vijana wanaobaleghe na wanaokaribia utu uzima, *tiba ya opioid agonist*, hasa methadone na buprenorphine, inaongoza kupungua kwa matumizi ya madawa ya kulevy, maambukizi ya VVU, na tabia za kuiweka katika hatari ya maambukizi miiongoni mwa watu wanaojidunga madawa. Pia ni salama na bora kwa wanawake wajawazito (inafaa miiongoni mwa

watu wazima).<sup>72</sup> Mipango ya kina ya kupunguza madhara, ikiwa ni pamoja na mipango ya kubadilisha sindano, usambazaji wa kondomu, tiba ya kemikali ya agonist na huduma ya kijamii, mipango ya uingiliaji kati mionganoni mwa vijana wenyе umri sawa, na ushauri kuhusu jinsi ya kupunguza hatari pasipo kuwahukumu, yaweza kupunguza tabia zinaochangia kusambaa kwa VVU mionganoni mwa watu wanaojidunga madawa ya kulevyia (*inafaa mionganoni mwa watu wazima*).<sup>73</sup>

Kuhimiza matumizi ya kondomu na tabia zingine za kujikinga ni muhimu mionganoni mwa vijana wanaotumia madawa ya kulevyia. Mbinu zinazohimiza tabia za kujikinga ni pamoja na elimu ya rika mionganoni mwa wanawake wanaotumia madawa ya kulevyia na wanawake wanaoshiriki ngono na wanaume wanaotumia madawa ya kulevyia (*inafaa mionganoni mwa watu wazima*).<sup>74</sup> Vikundi ambavyo vimegawanywa kwa jinsia na maumbile mionganoni mwa wapenzi wanaotumia dawa za kuelvyia pia vyaweza ongeza matumizi ya kondomu na kuongezeka kwa kujidunga sindano ya madawa kwa usalama (*inafaa mionganoni mwa watu wazima*).<sup>75</sup> Kutoa huduma za kupimwa na kushauriwa kuhusu VVU bila malipo kwa wanawake wanaotumia madawa ya kulevyia ni mbinu inayoonyesha matumaini ya kupunguza tabia zinazoongeza hatari ya kusambaa kwa VVU.<sup>76</sup>

### III. Utekelezaji na Mapengo ya Utafiti Mionganoni Mwa Vijana Wanaobaleghe

Kuingilia kati ambazo zinajenga mazingira mema na huduma za kutosha na zinazofikiwa kwa urahisi, zinawawezesha vijana wanaobaleghe kupata ufahamu na rasilmali za kujilinda pamoja na wapenzi wao.

Hata hivyo, baado kunasalia mapengo ya utekelezaji na utafiti. Kwa ujumla, mipango madhubuti lazima ipanuliwe ili kuwafikia vijana wenyе umri wa kubaleghe zaidi, hasa wale wamepuuzwa zaidi kama walio katika umri wa mapema wa kubaleghe, vijana walio nje ya shule, vijana wanaoishi na maradhi ya VVU, vijana wasio na makao, na wanaoishi katika sehemu za mashambani.<sup>77</sup> Mapengo yafuatayo yamejitokeza kutokana na tathmini ya kina ya maandiko.

#### Kiwango cha kijamii...

Sera wazi na sheria zakusaidia kwa habari na huduma, zinahitajika ili kupunguza hatari ya maambukizi ya VVU mionganoni mwa vijana.<sup>78</sup> Sheria na masharti yanayowazua vijana kufikia huduma, kama vile idhini ya wazazi, umri, na hali ya kindoa, sharti lazima kupitiwa upya na kufanyiwa marekebisho.<sup>79</sup> Sheria zinazozua ndoa katika umri mchanga zinapaswa kutungwa na kutekelezwa.<sup>80</sup> Juhudi zilizofaulu

za kuongeza kiwango cha elimu mionganoni mwa wasichana, hasa kwa shule ya upili, lazima zipanuliwe.<sup>81</sup>

#### Kiwango cha jumuia...

Mipango ya kuingilia kati inahitajika ili kupunguza visa vya ngono na ndoa zinazovuka vizazi,<sup>82</sup> pamoja na kuondoa kutumia nguvu kwa ngono na ubakaji wa wanawake, wasichana, wavulana, na wanaume. Jitihada zinahitajika ili kujenga kuelewa katika jamii kwamba dhuluma dhidi ya watu wazima na watoto hazikubaliki, kuimarisha mifumo ya kuwalinda watu wazima na watoto kisheria, na kubuni kutekeleza huduma zinazofaa za kuwalinda watu wazima na watoto katika mataifa yanayoendelea,<sup>83</sup> kuunganisha mipango ya VVU na ile inayoangazia dhuluma za kijinsia, ikiwa ni pamoja na dhuluma za kimpenzi mionganoni mwa watoto na tiba ya kuzuia maambukizi ya VVU (PEP).<sup>84</sup>

Katika sehemu zilizo na viwango vya juu vya matumizi ya madawa ya kupitishiwa kwenye mishipa, mbinu za kuingilia kati zinahitajika ili kuimarisha ufikiaji wa tiba ya dawa za methadone na buprenorphine—tiba thabiti ya kemikali ya agonist ili kutibu matumizi ya dawa ya kulevyia—vile vile mipango ya kubadilisha sindano/kusambaza.<sup>85</sup> Jitihada zinahitajika za kuondoa tabia za kuwazuilia kwa nguvu wanaotumia madawa ya kulevyia, na badala yake kuwapa watu wanaojidunga madawa (PWID) huduma ya kujikinga na kupimwa virusi vya UKIMWI na tiba ya kupambana na hali ya kutegemea madawa ya kuelvyia, kwa kutoa huduma za tiba na wataalamu wa kiafya.<sup>86</sup> Wasichana katika umri wa kubaleghe na ambao wanatumia dawa za kujidunga wanahitaji mipango ya kupunguza hatari ya maambukizi ili kufikia mahitaji yao.<sup>87</sup> Vile vile, taarifa na huduma za kisiri za kujikinga kutokana na maambukizi ya VVU, zinapaswa kupatikana kwa urahisi mionganoni mwa watu wanaojidunga dawa (PWID) na ambao wanaopokea tiba dhidi ya matumizi ya madawa ya kulevyia.<sup>88</sup> Mipango ya kuingilia kati inapaswa kuwafahamisha vyema wanawake pamoja na wapenzi wao kuhusu hatari ya kuambukizwa maradhi ya VVU kuitia ngono, vile vile kuitia kujidunga dawa za kulevyia.<sup>89</sup> Wanawake wanaotumia dawa za kulevyia kwa kujidunga wanapaswa kufikia huduma za dhuluma dhidi ya wanawake, na matumizi ya upangaji uzazi na kondomu kwa wakati mmoja, na mbinu tabiti za upangaji uzazi, na afya ya uzazi.<sup>90</sup> Idadi kubwa ya mapengo haya imetambuliwa mionganoni mwa watu wazima lakinia pia inashuhudiwa mionganoni mwa vijana wanabaleghe. Elimu ya masuala ya ngono na mipango ya kuhimiza matumizi ya kondomu zinapaswa kuzingatia vichocheo tofauti baina ya wanaume na wanawake vinavyowafanya wajihusisha na ngono bila kinga,<sup>91</sup> na mipango ya kukabiliana na VVU inapaswa kuwa thabiti katika harakati za kuwahusisha wanaume na wanawake kwa kuongeza lengo la usawa wa kijinsia.<sup>92</sup> Kuongezeka kwa mafunzo zaidi kwa walimu na sera zilizowazi za elimu ya kujamiihana na kutoa elimu bora

ya UKIMWI, zinatakitikana.<sup>93</sup>

Hatua inapaswa kuchukuliwa ili kuimarisha ufahamu wa vijana wanaobaleghe kuhusu lini na wapi wanaweza fikia huduma za kifaya, ikiwa ni pamoja na huduma ya upangaji uzazi na kondomu.<sup>94</sup>

Mipango hususan ya kuingilia kati inahitajika kwa dharura ili kuimarisha ufkiaji wa kondomu za wanawake. Vile vile kutoa elimu na mafunzo kuhusu jinsi ya kuzitumia kama chaguo ziada za kondomu.<sup>95</sup> Watoaji bidhaa hizi wanapaswa kupokea mafunzo ili kuhamasisha matumizi ya kondomu za wanawake<sup>96</sup> na kuhusu matumizi ya kondomu za kike na kujadili kujamiihana kwa furaha na kujadiliana na vijana wanaotumia huduma za afya ya uzazi kuhusu suala la ujinsia na raha ya matumizi haya.<sup>97</sup> Mipango hii inapaswa kuendelea kuhimiza tabia ya kujikinga, kama vile matumizi ya kondomu, pamoja na kutahiriwa kwa wanaume.<sup>98</sup> Mipango kuhusu kutahiri wanaume inapaswa kuwapa wanawake na wasichana, vile vile wanaume na wavulana ufahamu wa kina kuhusu faida na hatari za shughuli za kutahiriwa kwa hiari miiongoni mwa wanaume kutokana na sababu za kimatibabu,<sup>99</sup> na kushirikisha mafunzo ya kijinsia kwa wanaume vijana.

Hatua lazima zichukuliwe ili kufanya upimaji wa VVU na nasaha kuhusu UKIMWI (HTC) zinapatikana kwa urahisi na kufikiwa na vijana wanaobaleghe,<sup>100</sup> na kuwashakikishia usiri wa matokeo baada ya kupimwa VVU.<sup>101</sup> Pia hatua zaidi zinapaswa kuchukuliwa kuhakikisha mikakati na mada mwafaka katika utekelezaji wa HTC, pamoja na taarifa za kina kuhusu jinsi ya kufikia tiba na kupunguza hatari ya maambukizi.<sup>102</sup> Utekelezaji wa itifaki za viwango vinavyohitajika ili kupunguza hatari ya ushurutishaji wa watoaji huduma katika harakati za kupima maradhi ya VVU, hasa inapohusisha shughuli ya upimaji na ushauri iliyoshawishiwa na wanaotoa huduma hiyo.<sup>103</sup>

## Kiwango cha uhusiano...

Kubadilisha kanuni za kijinsia ambazo zinaweza ongeza hatari ya maambukizi ya VVU, kama vile zinazoamuru kushiriki ngono na watu kadha, kutumia nguvu, au kunywa pombe kupita kiasi kwa wanaume na kupuuza masuala ya kijinsia, unyenyekevu, na tabia ya wanawake na wasichana kutegemea wanaume ni changamoto.<sup>104, 105</sup> Mipango ya kuingilia kati iliyotathiminiwa zaidi inahitajika na mipango iliyopo inapaswa kupanuliwa. Mipango ya kuingilia kati inahitajika ili kukomesha chuki dhidi ya mabasha, suala ambalo laweza pelekea wanaume wanaoshiriki ngono na wanaume wenzao kuwa na uhusiano wa ngono na wanawake<sup>106</sup> —suala nyeti kwa vijana kwa sababu utambulisho na ugunduzi wa kijinsia huanza utotoni na katika umri wa kubaleghe. Upanuzi na uimarishaji wa mipango inayotoa fursa za kiuchumi kwa wanawake na wasichana unahitajika

ili kuongeza uwezo wao wa kukataa kushiriki ngono bila kinga ili kupata mahitaji ya kiuchumi.<sup>107</sup> Mbinu zinazopunguza muda wa kusafiri na/au kuhakikisha ufkiaji rahisi na salama wa usafiri, huenda ukapunguza hatari ya dhuluma za kijinsia miiongoni mwa wasichana wanaobaleghe.<sup>108</sup>

Hatua za kuingilia kati zinahitajika kwa dharura ili kupunguza visa yya kuwa na wapenzi wengi—hasa katika maeneo yanayoaminika kuwa na idadi ya chini ya watu walio na VVU, huku wanawake wakitarajiwa kuwa waaminifu, na wanaume wakiruhusiwa kuwa na wapenzi kadha.<sup>109</sup>

## Kiwango cha kibinafsi...

Jitihada kubwa zinatakitikana za vijana kubinafsi hatari za maambukizo ya VVU<sup>110</sup> na kwa vijana katika umri wa kubaleghe kupunguza kukubalika kwa dhuluma za kijinsia na unyanyapaa dhidi ya watu wanaoishi na VVU.<sup>111</sup> Jitihada zahitajika za kuwaelimisha wasichana kati ya miaka 8 na 14 kuhusu hedhi, kubaleghe, na ufahamu msingi kuhusu VVU.<sup>112</sup>

Hatua zaidi zinahitajika kuwasaidia wasichana mayatima na watoto wanaoishi katika mazingira magumu kupunguza tabia za ngono hatarishi na kuwanlinda na vurugu za kijinsia.<sup>113</sup>

Mipango ya msaada, ikiwa ni pamoja na kutoa ushauri nasaha, zinahitajika kwa ajili ya watoto walioachwa mayatima kutokana na UKIMWI, na walezi wao kukabiliana na huzuni, kutengwa kijamii, na unyanyapaa.<sup>114</sup> Jitihada hizi zinapaswa kuwashughulisha wanaume kuhusika kwa matibabu ya watoto na huduma kwa mayatima.<sup>115</sup>

Kwa vijana wanaokaribia utu uzima na wanaojihusisha na biashara ya ngono (angalia ufanuzi wa umoja wa Mataifa), taarifa msingi kuhusu huduma zinazohusiana na VVU, kama vile maeneo ya kupata kondomu na huduma za siri za kupimwa VVU, bado vinahitajika.<sup>116</sup> Umakini kwa utafiti na utekelezaji ni muhimu kwa maendeleo ya ushahidi wa kina na msingi wa mikakati madhubuti kuzuia VVU miiongoni mwa vijana.



Photo by: Dietmar Temps

## IV. Kuendelea Mbele: Mazingatio ya Kuongeza Mipango Yenye Mafanikio Miiongoni Mwa Vijana Wanaobaleghe

Kuimarisha mbinu za kujikinga kutokana na maambukizi Kuongeza mbinu za kujikinga kutokana na maambukizi ya VVU ni muhimu katika harakati za kuwafikia vijana wanaobaleghe. Kuna jitihada kadha chache ambazo zimethibitishwa kuwafikia vijana. Lakini iwapo hazitaongezwa, hazitakuwa na matokeo dhidi ya athari zinazotokana na kusambaa kwa VVU. Katika uchambuzi wa utafiti kuhusu jinsi ya kuzuia kusambaa kwa VVU katika kipindi cha miaka 25 iliyopita, Rotheram-Borus, et al. (2009) aliangazia kuwa "mbinu thabiti katika harakazi za kuzuia kuenea kwa VVU, zinahitaji mchanganyiko wa mikakati ya kitabia, athari za kimazingira kwa binadamu, na muundo." Shughuli za kuimarisha mipango iliyothibitishwa hazijaridhisha. Watafiti wa mbinu za kujikinga wanatambua kuwa changamoto ya sasa ni "kubuni upya jinsi mipango ya kuzuia virusi hivi itagharamia nafuu, muhimu, ukweli, kufanyiwa majoribio, na kusambazwa kwa njia isiyogharimu fedha nyingi, muhimu, yenye uhalisi na kuhimiliwa."<sup>117</sup>

Kumekuwa na tofauti baina ya vijana wanaobaleghe ulimwenguni, na mipango iliyofaulu yaambatana na mazingira. Hata hivyo, maelezo mbali mbali yanaonyesha kuwa kuzuia usambazaji wa VVU miiongoni mwa vijana wanaobaleghe kunahitaji maoni ya kina na yanayohusisha sekta mbali mbali huku jumbe sawa zikirudiwa mara kwa mara kutoka kwa vyanzo vingi. Masuala kadha muhimu yanahitajika ili kuimarisha mipango hii (tazama Kijisanduku 1).

